

## HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

### MRADI WA HIFADHI YA MSITU ASILI NA UFUGAJI NYUKI KATIKA KIJIJI CHA IBOJA

Mradi wa ufugaji nyuki na uhifadhi katika msitu wa kijiji cha Iboja. Mradi huu ulianzishwa kiasili kwenye hifadhi hii ya kijiji cha Iboja mwaka 1984 na unaendeshwa kwa kufuga nyuki kiasili na kikundi cha ujasiriamali kiitwacho **Ufugaji Nyuki ni Ajira**. Lengo la mradi ni kuboresha uhifadhi wa uoto wa asili pamoja na kujipatia kipato kwa wanakikundi. Msitu huu wa hifadhi una ukubwa wa ekari 100 sawa na Hekta 40.47 na thamani yake inakadiriwa kuwa Tshs 125,100,000.

Kikundi kina jumla ya wanachama kumi na sita (16) na mizinga ya nyuki 80, ikiwemo 20 ya kisasa na 60 ya kiasili. Thamani ya mradi huu wa ufugaji nyuki ni Tsh 4,000,000. Uzalishaji wa **asali na nta** unafanyika mara mbili kwa mwaka, yaani mwezi Mei hadi Julai na Septemba hadi Oktoba.

Mavuno ya **asali** ni lita 400 na **nta** kilo 50 kwa mwaka, ambapo kikundi kinapata mapato ya Tshs 2,500,000 kwa mwaka.

### MRADI WA HIFADHI YA MSITU ASILI NA UFUGAJI NYUKI KATIKA KIJIJI CHA IBOJA





## **HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

**MRADI WA MAJI YA BOMBA KATIKA VIJJI VYA IBOJA, KAYENZE NA KUNDIKILI**  
mradi wa maji ya bomba unaohudumia vijiji vitatu vya Iboja, Kayenze na Kundikili. Mradi huu unahudumia wakazi wa kawaida wapatao 7,286 pamoja na taasisi 7, kati ya hizo 6 ni za umma na moja ni ya dini. Taasisi hizo ni Kituo cha Afya Ukune, S/M Iboja, S/M Buzabi, S/M Kayenze, S/M Ukune na Shule ya bweni ya Sekondari ya Dakama na misheni ya wakatoliki Iboja

Chanzo cha maji ni kisima kirefu chenye urefu wa mita 82 kutoka juu ya ardhi na chanzo hicho kina uwezo wa kutoa lita 12,000 kwa saa.

Mradi huu una matenki mawili ya maji, moja lina ujazo wa lita 45,000 na la pili lina ujazo wa lita 100,000

Upatikanaji wa maji katika maeneo haya utasaidia sana maendeleo ya wakazi wa kawaida kwa kunywa maji safi na salama kwa afya zao. Mradi unasimamiwa na

### **JUMUIYA YA WATUMIAJI MAJI YA IBOJA, KAYENZE NA KUNDIKILI (KAIBOKU)**

Mradi umegharimu jumla ya shilingi **860,834,487/=** kwa mchanganuo ufuatao: -

- Michango ya wananchi shilingi 2,788,947.00
- Halmashauri ya Wilaya shilingi 20,927,940.00
- Mchango wa Serikali Kuu shilingi 837,117,600.00

**MRADI WA MAJI YA BOMBA KATIKA VIJJI VYA IBOJA, KAYENZE NA KUNDIKILI**



## **HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

### **UJENZI WA JENGO LA OFISI ZA MPITO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

jengo la ofisi za mpito za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ambalo ujenzi wake unaendelea.

Mradi huu wa jengo la ofisi ulianza tarehe 29 April, 2017 kwa kutumia utaratibu wa Halmashauri kufanya manunuzi yenyewe (Force Account) na kwa sasa upo kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji.

Mradi huu hadi kufikia hatua hii umegharimu fedha kiasi cha shilingi milioni mia moja themanini na tisa (189) kati ya milioni mia mbili (200) zinazotarajiwa kutumika hadi kukamilisha ujenzi, zikiwa ni fedha kutoka Serikali Kuu.

Ni imani yetu kuwa baada ya jengo hili kukamilika watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu wataweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Ujenzi wa jengo hili utatatia changamoto kubwa ya uhaba wa ofisi za watumishi uliokuwa unaikabili Halmashauri tangu ilipohamia katika eneo lake la Makao Makuu Julai,2016. Ni imani yetu kuwa wananchi sasa watapata huduma katika mazingira mazuri kutokana na ofisi za Halmashauri kuboreshwa.

**UJENZI WA JENGO LA OFISI ZA MPITO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**



**JENGO LA OFISI ZA MPITO HALMASHAURI YA USHETU**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

### UJENZI WA BARABARA YA MITONGA

barabara ambayo imefanyiwa matengenezo ya kawaida (Routine Maintenance) kwa ajili ya kuboresha mtandao wa mawasiliano kati ya vijiji vya kata za Bukomela na Nyamilangano kupitia kijiji cha Mitonga. Barabara hii ina urefu wa kilomita 12 na matengenezo ya barabara hii yamegharimu kiasi cha shilingi **milioni arobaini na mbili na laki tisa (42,900,000)**. Baada ya maelezo haya tunaomba uone matengenezo ya barabara yanayofanywa na mitambo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu



## **HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

### **MRADI WA UJENZI JENGO LA WAGONJWA WA NJE (OPD) KATIKA ZAHANATI YA BUKOMELA**

jengo la wagonjwa wa nje (OPD) katika kijiji cha Bukomela ambalo limejengwa kuboresha huduma za afya katika kata ya Bukomela. Kabla ya kujengwa jengo hili tumekuwa tukilitumia jengo lililo pembeni kidogo lililojengwa zamani na ambalo kwa sasa halikidhi viwango vya majengo ya kutolea huduma za afya. Baada ya kuona changamoto hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Bukomela na Serikali kuu tumejenga jengo jipya na la kisasa kwa gharama ya shilingi 75,000,000/= kwa mchanganuo ufuatao

- Wananchi shilingi 3,000,000
- Halmashauri shilingi 43,900,000
- Serikali Kuu shilingi 28,100,000

Msukumo wa ujenzi wa jengo hili ulitokana na hadhi ya nyota sifuri (0) ya jengo la awali baada ya tathimini ya Lipa kwa Matokeo (RBF) iliyofanyika mwaka 2015

Aidha zahanati hii ina uwezo wa kuhudumia zaidi ya watu 7,171 waishio kata ya Bukomela yenye vijiji Vinne na vijiji vya kata za jirani za Nyamilangano, Kinamapula na Uyogo. Jengo hili lina uwezo wa kuhudumia akinamama 2 kujifungua kwa wakati mmoja, pia kupumuzisha wagonjwa 4 kwa siku. Zahanati hii ina jumla ya watumishi 5; Tabibu msaidizi 1, wauguzi wasaidizi 2 na wahudumu wa afya 2



**JENGO LA WAGONJWA WA NJE (OPD) ZAHANATI YA BUKOMELA**



**MWONEKANO WA JENGO LA WAGONJWA WA NJE (OPD) ZAHANATI YA BUKOMELA**

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

### **MRADI WA UONGEZAJI THAMANI YA MAZAO KATIKA KIWANDA CHA KUSINDIKA ALIZETI KATA YA UYOGO**

mradi wa kuongeza thamani ya mazao katika kiwanda cha kusindika alizeti unaomilikiwa na mjasiriamali Ndg. Bunga Belenganyi.

Kiwanda hiki, kimeanzishwa mwaka 2010 na kimeendelea kuboreshwa ili kuitikia Sera ya Serikali ya awamu ya Tano inayohimiza uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda katika maeneo mbalimbali nchini ili kufikia malengo ya uchumi wa kati. Kiwanda hiki, kilianzishwa kwa lengo la kutumia rasilimali za kilimo zinazopatikana ndani ya Halmashauri ya Ushetu pamoja na kutoa ajira na lishe bora kwa jamii na mifugo. Tangu kuanzishwa kwake, kiwanda kidogo kimezalisha na kufungasha jumla ya **lita 143,200** za mafuta na mashudu ya alizeti **tani 572,800**.

Mradi huu wa kiwanda cha kusindika alizeti hadi kukamilika utagharimu kiasi cha shilingi **43,500,000**. Mchango wa Halmashauri katika mradi huu ni ushauri wa kitaalamu

Eneo la viwanda lililotengwa kwa kata hii ya Uyogo ni ekari kumi

**KIWANDA CHA KUSINDIKA ALIZETI KATA YA UYOGO**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

**T MRADI WA KUZUIA UPOTEVU WA MAZAO BAADA YA MAVUNO, KIJJI CHA  
IBELANSUHA**

Mradi wa kuzuia upotevu wa mazao baada ya mavuno kijiji cha Ibelansuha. Kijiji hiki ni miongoni mwa vijiji 46 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ambavyo vinatekeleza mradi huu. Mradi huu unatekelezwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa shirika la "HELVETAS SWISS INTER COOPERATION".

**Shughuli za mradi zilizofanyika mpaka sasa ni: -**

1. Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 21 ambao hufundisha wakulima mbinu za hifadhi bora ya mazao vijijini.
2. Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji VICOBA 9 kwa ajili ya kuwafundisha wakulima mbinu za kupata vifaa vya hifadhi ya mazao mfano vihenge (metal silo), mifuko ya *PICS* na *Agro-Z*.
3. Kutoa mafunzo kwa mafundi mchundo 9 kwa ajili ya kutengeneza vihenge (metal silo).

Hadi sasa jumla ya wakulima 3,255 wamepata mafunzo ya hifadhi ya mazao, kati ya hao wakulima 655 wamejiunga katika vikundi vya VICOBA na 2,600 katika vikundi visivyo vya VICOBA.

Fundi mchundo mmoja wa vihenge (metal silo) kwa kila kata amepatiwa mafunzo ya utengenezaji wa vifaa hivyo. Hadi sasa vihenge (metal silo) 125 vyenye ujazo mbali mbali vimetengenezwa na kukopeshwa kwa wakulima kupitia vikundi vyao. Jumla ya mifuko 2055 ya *Pics* ya kuhifadhia nafaka na mikunde imeunuliwa na wakulima.

Thamani ya vihenge (metal silo) vilivyoko mbele yako ni jumla ya shilingi 1,553,500/= ambazo ni mchango wa Halmashauri na zitakopeshwa kwa wakulima na fedha zitakazorejeshwa zitaendeleza mradi kwa kuwakopesha wakulima wengine.

**VIHENGE VYA UJAZO TOFAUTI TOFAUTI KIJJI CHA IBELANSUHA**



## **HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

### **UJENZI WA JOSHO LA KUOGESHEA MIFUGO LA KATA YA ULOWA**

Mradi wa ujenzi wa joshu la kuogeshea mifugo la wafugaji wa kata ya Ulowa ambalo limejengwa na wafugaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

Kata ya Ulowa ina jumla ya ng'ombe 14,289 Mbuzi 5,307 na kondoo 572 ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakisumbuliwa na magonjwa yaenezwayo na kupe hususani ndigana kali (ECF), ndigana baridi (Anaplasmosis), mkojo damu (Babesiosis), maji moyo (Heart water) na ukurutu (Mange).

Mradi huu wa ujenzi wa joshu umeanza rasmi mwezi Aprili, 2017 na kwa sasa umefikia hatua ya mwisho na leo unazinduliwa. Hadi kukamilika kwa mradi huu jumla ya Tshs 27,500,000/= zimetumika kwa mchanganuo ufuatao: -

- Mchango wa Serikali Kuu ni Shilingi 15,000,000/=
- Mchango wa jamii ya wafugaji ni shilingi 12,500,000/=

**JOSHO LA KUOGESHEA MIFUGO LA KATA YA ULWA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**  
**MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VINANE (8) VYA MADARASA OFISI NNE (4)**  
**ZA WALIMU NA MATUNDU ISHIRINI (20) YA VYOO KATIKA SHULE YA**  
**MSINGI NONWE**

Mradi wa ujenzi wa vyumba Vinane vya madarasa, ofisi Nne za walimu na matundu ishirini ya vyoo katika shule ya Msingi Nonwe iliyoko katika kata ya Ubagwe.

Shule ya msingi Nonwe ina jumla ya wanafunzi **2273** (wav **1173** was **1100**). Idadi hii ni kubwa sana inayohitaji miundo mbinu ya kutosha.

Mradi huu ulianza kujengwa Tarehe 26/9/2016 na umekamilika juni mwaka huu 2017 na leo tunatarajia utufungulie rasmi.

Mradi huu umegharimu jumla ya shilingi za kitanzania milioni mia moja themanini na mbili (182,000,000/=) elfu, na umejengwa kwa pesa ya serikali kupitia mpango wa **LIPA KULINGANA NA MATOKEO (P4R)**

Ujenzi wa mradi huu umekamilika chini ya usimamizi wa viongozi na wataalam toka ngazi ya Halmashauri kwa kushirikiana na mafundi wenyeji (Local fundis), serikali ya kijiji, kamati ya shule, na walimu wote kwa ujumla.

Mradi huu pia unajumuisha utengenezaji wa dawati 120.

Kutokana na usimamizi na ushauri bora wa kitaalam imewezekana majengo haya kuwa na ofisi nne, pia vyoo vya ndani matundu manne (4) kwa ajili ya matumizi ya walimu

Kufunguliwa kwa majengo haya kutapunguza hali ya mrundikano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa unaosababishwa na upungufu wa vyumba vya madarasa na hivyo kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

**VYUMBA VINANE (8) VYA MADARASA OFISI NNE (4) ZA WALIMU NA MATUNDU ISHIRINI  
(20) YA VYOO KATIKA SHULE YA MSINGI NONWE**



**MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VINANE (8) VYA MADARASA**



**BAADHI YA VYOO KATI YA ISHIRINI (20) KATIKA SHULE YA MSINGI NONWE**



## HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

### VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA AMBAVYO VINAPATIWA MIKOPO TOKA MFUKO WA VIJANA NA WANAWAKE

Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilifanikiwa kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa vikundi vya wanawake na vijana 33 yenye thamani ya shilingi 81,500,000 sawa 54.2% ya lengo la mwaka la kutoa shilingi 150,490,320.

Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu imetoa mikopo yenye thamani ya Shs. 31,000,000/= kwa vikundi 9. Kati ya fedha hizo shilingi 20,000,000/= ni kwa ajili ya vikundi vitano (5) vya vijana na shilingi 11,000,000/= ni kwa ajili ya vikundi vinne (4) vya wanawake.

#### 1: VIKUNDI VYA VIJANA

NA	JINA LA KIKUNDI	KIJIJI	KATA	KIASI CHA MKOPO
1	Kikundi cha Kilimo Jembe	Igunda	IGUNDA	3,000,000
2	Wachapakazi	Imalabupina	NYANKENDE	3,000,000
3	Kikundi cha Mshikamano	Kalama	KINAMAPULA	3,000,000
4	Upendo	Kangeme	ULOWA	6,000,000
5	Iboja Ufundi	Iboja	UKUNE	5,000,000
				<b>20,000,000</b>

#### 2: VIKUNDI VYA WANAWAKE

NA	JINA LA KIKUNDI	KIJIJI	KATA	KIASI CHA MKOPO
1	Kikundi cha Wapendanao Misayu	Misayu	UBAGWE	3,000,000
2	Kikundi cha Upendo wanawake	Idahina	IDAHINA	3,000,000
3	Upendo Daima	Itumbili	CHAMBO	2,000,000
4	Kikundi cha Urafiki	Ididi	NYAMILANGANO	3,000,000
				<b>11,000,000</b>